https://maktaba.tetea.org

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
# MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A

**686 VITENDO VYA KUJIFUNZA KISWAHILI**

**Muda:Saa 3** **Mwaka: 2020**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na maswali **mawili (2)** kutoka kila sehemu B na C.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B na C zina alama **thelathini (30)** kila moja.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** kwenye chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

2 010621 100018



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Orodhesha zana nne atakazotumia mwalimu kumfundisha mtoto stadi ya kusimulia.

2. Chambua kwa kifupi changamoto nne za kutumia mbinu ya igizo katika kufundisha hatua za ukuaji wa lugha kwa mtoto.

3. Bainisha njia nne anazoweza kuzitumia mtoto ili kuweza kutambua maneno katika kujifunza lugha.

4. Taja mazoezi manne ya kulainisha viungo vya mtoto ili kumwandaa kujifunza stadi za awali za kuandika.

5. Eleza kwa kifupi jinsi mtoto anavyoweza kutumia lugha katika kujenga mahusiano mazuri katika jamii.

6. Fafanua kwa kifupi matendo manne ambayo mzazi anaweza kuyafanya ili kukuza lugha kwa mtoto wa miaka sifuri hadi miwili.

7. Onesha hatua nne za kufuata wakati wa kufundisha kuandika herufi '**b**'.

8. Orodhesha zana nne ambazo mwalimu anaweza kutumia kumfundisha mtoto kutamka maneno.

9. Fafanua kwa kifupi jinsi mazingira yafuatayo yanavyochangia katika kujifunza stadi za awali za kusoma kwa mtoto:
   (a) Mazingira ya nyumbani
   (b) Mazingira ya shuleni

10. "Mbinu za kufundishia stadi ya kuandika kwa watoto wa darasa la awali lazima ziwe na sifa stahiki." Ainisha sifa nne.

## SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

11. "Mwalimu anapomfundisha mtoto stadi za awali za kuzungumza anaweza kukutana na changamoto nyingi." Thibitisha kauli hiyo kwa hoja tano.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

12. Fafanua kwa kina mambo matano yanayoweza kuathiri ujifunzaji wa stadi za awali za kusoma kwa mtoto katika mazingira ya shuleni.

13. Chambua faida tano za kutumia zana za kufundishia wakati wa kufundisha stadi ya kuandika kwa darasa la awali.

**SEHEMU C (Alama 30)**

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

14. Chambua kwa kina hatua tano utakazozifuata unapomfundisha mtoto kusoma neno '**baba**' kwa kutumia mbinu ya onesho.

15. Bainisha matendo matano atakayoyafanya Mwalimu kumzoesha mtoto kusikiliza kwa makini.

16. Eleza matayarisho manne ya mwanzo yanayohitajika ili kumfundisha mtoto stadi za awali za kuandika.



Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org